MASWALI & MAJIBU 21

UTARATIBU, SIFA NA VIGEZO VYA UTOAJI MIKOPO KWA 2018/2019

Tunawawezesha Wahitaji

1. Swali: Ninapaswa kufanya nini ili niweze kuanza kuomba mkopo kwa njia ya mtandao (OLAMS)?

Jibu: Soma mwongozo uliotolewa na Bodi ambao unapatikana katika tovuti ya Bodi (www.heslb.go.tz). Baada ya kuusoma Mwongozo, fungua mtandao wa maombi (www.olas.heslb.go.tz) ili ujisajili kwa kutumia namba yako ya mtihani wa kidato cha nne na mwaka uliofanya mtihani huo.

2. Swali: Baada ya kujisajili, napaswa kufanya nini?

Jibu: Baada ya kujisajili, utapata namba ya kumbukumbu (Control Number) kutoka kwenye 'screen' ambayo itakuwezesha kufanya malipo ya ada ya maombi ya TZS 30,000/= kwa njia ya benki au simu. Lipa mara moja tu!

Baada ya kulipa, utapokea ujumbe (sms) wa uthibitisho wa muamala wako utakaokuwezesha kuendelea na hatua inayofuata ya maombi kwenye 'My Application'. Jaza hatua kwa hatua.

3. Swali: Je, nikiingiza namba yangu isiyokuwa ya NECTA, mfano ya nje ya nchi, nitawezaje kuendelea kuomba mkopo?

Jibu: Wakati wa kujisajili, unatakiwa kuchagua kipengele cha 'Non-NECTA students' na kujaza kama inavyoelekezwa. Mfumo utakupatia namba ya kidato cha nne tofauti na ile uliyojaza ambayo itatambuliwa na Bodi. Namba hii mpya itatokana na ile namba iliyojazwa awali (isiyokuwa ya NECTA).

4. Swali: Inachukua muda gani fomu kufunguka baada ya kulipa?

Jibu: Fomu inafunguka mara tu malipo yanapokamilika. Fomu inapochelewa kidogo kufunguka, mwombaji anashauriwa kutoka (Sign out) na kujaribu kuingia tena (Sign in) katika mtandao ili aweze kuendelea na hatua zinazofuata.

5. Swali: Ikiwa nimelipa lakini sijapokea ujumbe wa kuendelea na maombi, nifanyeje?

Jibu: Unatarajiwa kupokea ujumbe mara tu muamala unapokamilika. Ikiwa hautapata ujumbe ndani ya saa moja (dakika 60) baada ya kufanya malipo, unashauriwa kuwasiliana nasi kwa namba ya simu +255 22 550 7910 au barua pepe helpdesk@heslb.go.tz

6. Swali: Nitanyaje ikiwa njia mojawapo ya kulipia mfano, CRDB, NMB, M-pesa, Airtel Money, Tigo-Pesa itanigomea kulipa na kuendelea?

Jibu: Kwa kuwa kuna njia zaidi ya moja ya kulipia, unashauriwa kuchagua na kutumia njia ya malipo ambayo ni rahisi kwako au inapatikana sehemu uliyopo wakati ukifanya malipo.

7. Swali: Nifanyeje iwapo nimesahau neno langu la siri (Password)?

Jibu: Utapaswa kubofya kiunganishi cha "Forgot Password?" na kisha utaelekezwa kwenye ukurasa husika na ambako utatakiwa kujaza anuani ya barua pepe uliyotumia wakati wa kujisajili. Baada ya hapo, utapokea kiunganishi kwa ajili ya kupata neno jipya la siri kupitia kwenye barua pepe yako.

8. Swali: Je, ni wapi nitahakiki cheti za kuzaliwa au kifo cha mzazi?

Jibu: Vyeti vya kuzaliwa na vifo vya wazazi lazima vihakikiwe na Wakala wa Usajili, Ufilisi na Udhamini (RITA) kabla havijapakiwa (uploaded). Kumbuka kuwa RITA watawasilisha kwa Bodi orodha ya vyeti vyote vilivyohakikiwa ili kuepusha udanganyifu.

9. Swali: Je kuna athari zozote ikiwa nimeambatanisha na kuwasilisha cheti ambacho hakijahakikiwa na RITA?

Jibu: Ndiyo. Maombi yako yatakuwa hayajakamilika na hivyo kutofikiriwa katika hatua ya upangaji mikopo. Unapaswa kuhakikisha nyaraka zote (siyo vyeti vya vifo au kuzaliwa tu) zinathibitishwa na mamlaka, taasisi au maafisa waliotajwa katika mwongozo.

10. Swali: Je, ikiwa kazi ya mzazi wangu haipo kwenye orodha iliyopo kwenye mtandao, napaswa kufanya nini?

Jibu: Chagua kipengele cha nyinginezo (others) kisha uitaje kazi ya mzazi/mlezi wako kwa kuiandika.

11. Swali: Kama sikuwahi kumfahamu mzazi wangu, nitajaza nini?

Jibu: Unatakiwa kujaza taarifa za mlezi au mtu mwingine anayekulea au kusimamia masuala yako ya Elimu. Ni lazima taarifa za mlezi au msimamizi zithibitishwe na Serikali ya Mtaa unakoishi. Kama mlezi anazo nyaraka rasmi za kukuasili (adoption document) nazo ziambatanishwe.

12. Swali: Je, nikikosea kwenye 'Applicant category' natakiwa kufanya nini?

Jibu: Ikiwa bado 'huja-print', unaweza kurekebisha kwa kurudi kwenye 'Applicant Category' na kuchagua kipengele sahihi. Iwapo umekamilisha maombi na ku-print fomu yako, unatakiwa kuandika barua ya kuomba kufanyiwa marekebisho, na kuituma HESLB kwa njia ya EMS. Barua hiyo iwe namba ya kidato cha nne yenye mwaka uliofanya mtihani huo.

13. Swali: Je, kama nimehitimu kidato cha sita au diploma mwaka 2018 na sijapata cheti nitaambatanisha nini?

Jibu: Unatakiwa kutaja namba ya mtihani wa kidato cha sita ambayo itatumika kuhakiki matokeo kutoka mamlaka husika. Kwa mhitimu wa diploma, unaweza kuambatanisha waraka wa matokeo (transcript).

14. Swali: Kama mwaka jana au kabla nilikuwa na umri chini ya miaka 30, je mwaka huu naweza kuomba mkopo?

Jibu: Kwa mwaaka wa masomo 2018/2019, umri wa juu wa mwombaji ni miaka 33. Umri umeongezwa kutoka miaka 30 hadi 33 ili kuongeza wigo wa wanufaika wa mikopo.

15. Swali: Iwapo niliwahi kupata mkopo zamani na nikaacha, kushindwa au ufukuzwa chuoni, nitaweza kupata mkopo mwingine?

Jibu: Iwapo uliwahi kuwa mnufaika wa mkopo wa fedha za Serikali, utapaswa kwanza kurejesha mkopo wote au angalau asilimia 25 ya deni lako kabla ya kufikiriwa kupata mkopo mwingine. Deni hili unaweza kulipata kwa kuomba ankara ya deni kwa barua pepe repayment@heslb.go.tz au kupiga simu 0766 852 610 au 0659 748 536 kwa Idara ya Urejeshaji wa Mikopo.

16. Swali: Kama nina wazazi wasio na uwezo, je niwasilishe uthibitisho wa aina gani ili kupata mkopo?

Jibu: Muombaji ambaye ana mahitaji maalum, ni lazima mahitaji na hali yake ithibitishwe na mamlaka husika kama Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na taasisi za aina hii. Taarifa za aina hii zitapekuliwa kuthibitishwa uhalisia na ukweli wake.

17. Swali: Kama nilikosa mkopo mwaka jana, nikalazimka kuahirisha masomo, natakiwa kuomba tena mkopo mwaka huu?

Jibu: Unaruhusiwa kuomba upya mkopo mwaka huu. Maombi yako yatapimwa kwa mwongozo na vigezo vya mwaka 2018/19. Unashauriwa usome mwongozo kwa makini na kuuzingatia. Aidha, kama unasoma mwaka wa pili au wa tat una kuendelea na una uhitaji wa mkopo, unaruhusiwa kuomba kwa kuzingatia vigezo vya mwaka huu.

18. Swali: Nitafanyaje nisipoweza kumfikia mtoa huduma kwa njia ya simu inayoonyeshwa kwenye mtandao?

Jibu: Kuna njia mbili za kuwafikia watoa huduma wa kitengo cha usaidizi (Helpdesk) Njia ya kwanza ni kwa simu +255 22 550 7910 na nyingine ni kwa barua pepe helpdesk@heslb.go.tz.
Unashauriwa kuwasilisha taarifa au changamoto husika kwa njia ya barua pepe ili wataalamu waifanyie kazi na kukupigia kama itahitajika. Kumbuka kuandika mawasiliano yako ya simu itakayotumika kukupigia.

19. Je, mwombaji atajuaje kama fomu yake ya maombi imejazwa kwa ukamilifu?
Mwombaji ana wajibu wa kuhakikisha nyaraka zote muhimu zimepakiwa kwenye mfumo wa maombi katika nakala laini. Nyaraka hizo ni pamoja na:

i. Picha ya mwombaji;
ii. Vivuli vya nakala za vyeti vya kitaaluma zilizothibitishwa na Wakili au Hakimu;
iii. Vivuli vya nakala za vyeti vya kuzaliwa au kifo zilizothibitishwa na RITA;
iv. Nakala za barua za ufadhili kutoka katika taasisi zinazotambulika;
v. Nakala ya fomu ya maombi iliyosainiwa na kugongwa muhuri na Serikali ya Mtaa, Hakimu au Wakili kama inavyoelekezwa;
vi. Aidha, nakala halisi ya fomu ya maombi inapaswa kusainiwa na mwombaji na mdhamini wake
vii. Maelezo ya kina yanapatikana katika mwongozo uliopo kwenye tovuti ya Bodi ya Mikopo (www.heslb.go.tz)

20. Swali: Fomu za maombi ya Mikopo zinawasilishwaje Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu?

Jibu: Baada ya kuzi-upload na kukamilisha fomu yake ya maombi, mwombaji a-print fomu iliyokamilika na kuituma kwenda kwa:

Mkurugenzi Mtendaji,
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu,
Barabara ya Sam Nujoma – Mwenge
S.L.P. 76068
14113 DAR ES SALAAM

21. Mwombaji atajuaje iwapo amepata mkopo?
Jibu: Baada ya Bodi kupokea, kuhakiki na kuchambua maombi ya Mikopo, majina ya Wanafunzi watakaofanikiwa kupangiwa Mikopo yatatangazwa kupitia tovuti ya Bodi ya Mikopo (www.heslb.go.tz) kabla ya kufunguliwa kwa vyuo vya elimu ya juu walikodahiliwa Wanafunzi husika.

Imetolewa na:
Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu
info@heslb.go.tz
Mei 2018

46 Barabara ya Sam Nujoma - Mwenge, S.L.P 76068, 14113
Dar es Salaam, Tanzania **Simu:** +255 22 2772432/2772433; **Nukushi:** +255 22 2700286; **Barua pepe:** info@heslb.go.tz; **Tovuti:** www.heslb.go.tz